

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),  
S.L. P. 20,  
MISUNGWI.

Simu: 255-732980745  
Nukushi: 255 732980745  
Barua Pepe: [ded@misungwidc.go.tz](mailto:ded@misungwidc.go.tz)  
Toouti: [www.misungwidc.go.tz](http://www.misungwidc.go.tz)

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**UFAFANUZI WA TAARIFA YA SHILINGI MILLIONI 432 ZA MAKUSANYO YA  
MAPATO YA NDANI ZINAZODAIWA KUTAFUNWA NA WATENDAJI  
ZILIZOCHAPISHWA KATIKA BAADHI YA VYOMBO VYA HABARI NCHINI.**

**Misungwi, Juni 3, 2020:**

Kufuatia taarifa zilizochapishwa kupitia vyombo mbalimbali vya Habari hapa nchini kuanzia tarehe 29 Mei, 2020 na kusambazwa kwa umma, kupitia Gazeti la Nipashe na Majira Times online (yote ya Mtandaoni) ya tarehe 29 Mei, 2020 ambayo kwa pamoja yalichapisha na kusambaza taarifa yenye kichwa cha habari, Nipashe *"Mongella atoa siku 14 watendaji waliopiga milioni 432 kurejesha,"* na Majira Times *"Waliotafuna milioni 432 za Halmashauri wahesabiwa siku"*.

Hivyo, inasemekana kuwa madai hayo yalinukuliwa na Waandishi wa Habari wakati wa hotuba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe, John Mongela wakati akizungumza katika Mkutano Maalum wa hoja wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Misungwi lililofanyika katika ukumbi wa MGS - Misungwi tarehe 28 Mei, 2020 na kuagiza fedha hizo zirejeshwe haraka.

Menejimenti ya Halmashauri inapenda kuufahamisha umma kwamba katika taarifa ya Mdhubiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2018/2019 ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, hakuna taarifa inayoonyesha kutafunwa ama wizi wa fedha wa shilingi milioni 432 za makusanyo ya ndani ya Halmashauri kama ilivyochapishwa katika baadhi ya vyombo vya Habari.

Kwa mantiki, hiyo taarifa zilizotolewa katika vyombo vya habari kuhusiana na kutafunwa kwa shilingi milioni 432 si za kweli kutokana na Menejimenti kujiridhisha pasipo shaka kutoka katika taarifa ya Mdhubiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2018/2019 ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi iliyowasilishwa

katika Baraza hilo na Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Mkoa wa Mwanza, ambaye aliipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi kwa kupata Hati safi kwa mwaka 2018/2019, sambamba na kuitaka Halmashauri kukamilisha mapungufu yaliyobainishwa katika ukaguzi huo na kuagiza kuwasilisha utekelezaji wa majibu ya hoja ambazo hazijafungwa,

Kutokana na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi imepata Hati safi (**Unqualified Opinion**) na hoja zote zilizotolewa na Wakaguzi nyingi zimefungwa na baadhi zipo katika hatua ya utekelezaji.

Kwa maelezo ya taarifa hii, naomba kuuthibitishia umma kwamba taarifa zilizochapishwa kwenye baadhi ya vyombo vya habari kuhusu Watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi kutafuna shilingi milioni 432, ambazo zinadaiwa kuwa ni fedha za makusanyo ya ndani na kusambazwa kwa umma hazikuwa sahihi na zenye lengo la kupotosha ukweli kwa umma na hazikuzingatia maadili ya uandishi wa Habari.

Naomba kuwasisitiza Wanahabari kuendelea kufuata na kuzingatia kanuni na sheria mbalimbali zinazosimamia masuala ya upatikanaji na utoaji wa habari hapa nchini ikiwemo sheria ya haki ya kupata taarifa ya mwaka 2016 ili kuweza kupata na kuchapisha taarifa na habari zinazolenga kujenga jamii na kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa ustawi wa taifa letu.

Imetolewa na:



Thomas Lutego  
**AFISA HABARI NA MAWASILIANO  
KITENGO CHA TEHAMA, HABARI, MAWASILIANO NA  
UHUSIANO (W) MISUNGWI**